

Kiango na Pishi ni nini (Mathayo 5:15)?

Kiango ni kifaa maalumu cha kushikilia au kuning'inzia taa, tazama picha, kwa jina lingine kinaitwa kinara. Na nilazima kinyanyuke au kiwe sehemu ya juu kidogo, ili kuruhusu mwanga wa hicho kilicho juu yake (yaani taa) kuangaza mahali pote.



Na Pishi ni bakuli dogo, au kapu ndogo. Tazama picha,



Hivi ni vifungu ambavyo utaweza kukutana na maneno hayo;

Mathayo 5:15 “Wala watu hawawashi taa na kuiweka chini ya pishi, bali juu ya kiango; nayo yawaangaza wote waliomo nyumbani”.

Marko 4:21 “Akawaambia, Mwaonaje? Taa huja ili kuwekwa chini ya pishi, au mvunguni? Si kuwekwa juu ya kiango?”

Luka 11:33 “Hakuna mtu awashaye taa na kuiweka mahali palipositirika, au chini ya pishi; bali huiweka juu ya kiango, ili

waingiao wapate kuuona mwanga”.

Soma pia *Luka 8:16*

Hivyo mpaka hapo tunaweza kupata picha sasa Bwana Yesu alimaanisha nini kutoa mfano huo, kuwa tunapoamua kuokoka hatupaswi kuuficha wokovu wetu, kuuweka chini ya bakuli bali ni sharti tuungaze kwa watu wote, kwanza kwa matendo yetu na pia kwa kuwahubiria ili kusudi kwamba wavutwe na wao katika wokovu tulionao.

Na ndio maana pale kwenye Mathayo 5:15 akamalizia na kusema..

16 “Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze mbele ya watu, wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni”.

Shalom.

Tazama maana nyingine ya maneno ya biblia chini.

Kiango na Pishi ni nini (Mathayo 5:15)?

Tafadhali washirikishe na wengine habari hizi njema, na pia kama utapenda tuwe tunakutumia mafundisho ya Neno la Mungu ya mara kwa mara kwa njia ya email yako au Whatsapp basi tutumie ujumbe kwenye namba hii +255693036618 au +255789001312

jiunge na channel yetu Kwa kubofya hapa >> WHATSAPP

Mafundisho mengine

Mada Nyinginezo:

Maana ya Mafarisayo Hupanua HIRIZI zao, na kuongeza MATAMVUA yao

GOGU NA MAGOGU, Katika biblia ni nani?

“Shinikizo” ni nini kibiblia, Na maana yake rohoni ni ipi?

Uga ni nini? Na kazi yake ni ipi kibiblia?

SIFONGO NA SIKI NI NINI?

Rudi nyumbani

Share on:
WhatsApp

Print this post